


**JEDWALI LA MAREKEBISHO LITAKALOWASILISHWA NA MHE. NAPE MOSSES
NNAUYE, WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
WAKATI WA KUSOMWA KWA MARA YA PILI KWA MUSWADA WA SHERIA YA
ULINZI WA TAARIFA BINAFSI WA MWAKA 2022**

(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 99(10))

Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi unarekebishwa kama ifuatavyo:

- A:** Kwa kuongeza maneno yafuatayo mara baada ya jina refu la Sheria:
“Imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.”;
- B:** Katika Ibara ya 3-
- (a) kwa kuongeza maneno “au mchakataji” mara baada ya neno “mkusanyaji” lililopo katika tafsiri ya msamiati “afisa ulinzi wa taarifa binafsi”;
 - (b) kwa kufuta maneno “au miamala ya kifedha ya mtu binafsi” yaliyopo mwishoni mwa aya (b) ya tafsiri ya msamiati “taarifa binafsi”;
 - (c) kwa kufuta maneno “hukumu za jinai” yaliyopo katika aya (a) ya tafsiri ya msamiati “taarifa binafsi nyeti” na badala yake kuweka maneno “miamala ya kifedha ya mtu binafsi”;
 - (d) kwa kuongeza maneno “au njia nyingine” mara baada ya neno “kielektroniki” lililopo katika tafsiri ya msamiati “usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi”;
- C:** Katika Ibara ya 4 kwa kuongeza maneno “ukusanyaji na” kabla ya neno “uchakataji” popote linapojitokeza katika Ibara hiyo;
- D:** Katika Ibara ya 7 kwa kuongeza maneno “na wachakataji” mwishoni mwa aya (a);
- E:** Katika Ibara ya 8(1) kwa kufuta maneno “ambacho kitakuwa” na badala yake kuweka maneno “ambayo itakuwa”;
- F:** Katika Ibara ya 22(1) kwa kuongeza maneno “ukusanyaji na” mwanzoni mwa aya (a);
- G:** Katika Ibara ya 24 kwa kufuta na kuandika upya maelezo ya pembeni kama ifuatavyo:
“Usahihi wa taarifa binafsi”;
- H:** Katika Ibara ya 27(1) kwa kufuta neno “kizembe” na badala yake kuweka maneno “kizembe au”;
- I:** Katika Ibara ya 28(1) kwa kuongeza maneno “kwa kipindi kilichoainishwa katika sheria zilizopo au” kati ya maneno “taarifa hizo” na “kwa kipindi”;
- J:** Katika Ibara ya 30(2) kwa kufuta neno “idhini” na badala yake kuweka neno “ridhaa”;



- K:** Katika Ibara ya 31(3) kwa kufuta maneno “muda mfupi” na badala yake kuweka neno “awali”;
- L:** Katika Ibara ya 37-
(a) kwa kuongeza maneno “au mchakataji” baada ya neno “mkusanyaji” kila linapotokea katika ibara ndogo ya (1); na
(b) katika ibara ndogo ya (2) kwa kuongeza maneno “au mwakilishi wa mhusika wa taarifa ikiwa mhusika ni mtoto au mtu asiye na akili timamu” mwishoni mwa aya (a);
- M:** Katika Ibara ya 39 kwa kufuta na kuiandika upya ibara ndogo ya (1) kama ifuatavyo:
“(1) Mtu yeyote atakayebaini kuwa mkusanyaji au mchakataji amekiuka misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Tume.”;
- N:** Katika Ibara ya 40 kwa kuongeza maneno “au mchakataji” mara baada ya neno “mkusanyaji”;
- O:** Katika Ibara ya 42 kwa kuongeza maneno “au mchakataji” mara baada ya neno “mkusanyaji” kila linapotokea katika Ibara ndogo za (1), (2), (3), na (4);
- P:** Katika Ibara ya 56(3) kwa kuongeza maneno “na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali” mara baada ya neno “aliyeteuliwa”;
- Q:** Katika Ibara ya 58(1) kwa kufuta neno “mchakati” na badala yake kuweka neno “mchakataji”; na
- R:** Katika Jedwali-
(a) katika aya ya 2 kwa kuongeza mara baada ya aya (d) aya ifuatayo:
“(e) kifo.”
(b) katika aya ya 4 kwa kufuta maneno “kutokamilika idadi ya wajumbe wakati wa kikao husika au kwa”.

Dodoma,
....., 2022

NMN
WHMTH